HOTUBA YA MWENYEKITI WA MUUNGANO WA JUMUIYA ZA HIFADHI YA WANYAMAPORI (CWMAC), NDUGU CHRISTOPHER MADEMULA KATIKA MKUTANO WA PAMOJA KATI YA JUMUIYA ZA MAENEO YA HIFADHI YA WANYAMAPORI TANZANIA (WMAs) NA WAWEKEZAJI KWENYE MAENEO YA WMAs, KATIKA HOTELI YA NAURA SPRINGS, ARUSHA - TAREHE 15 MACHI 2016

Wawekezaji katika Maeneo ya Jumuiya za Hifadhi ya Wanyamapori (WMAs),

Wawakilishi na Viongozi kutoka WMAs,

Wawakilishi kutoka ENGILITY/Mradi wa USAID PROTECT,

Wawezeshaji kutoka Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs),

Viongozi na watumishi wa Muungano,

Mabibi na Mabwana.

Awali ya yote, kwa niaba ya Uongozi wa Muungano napenda kuchukua fursa hii kuwakaribisha **WOTE** kwenye Dhima hii muhimu katika mustakabali wa maendeleo ya WMAs Tanzania. Kipekee naomba kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, **Profesa Jumanne Magembe** kwa kukubali kuja kutufungulia mkutano wetu kwani tunatambua unamajukumu mengi ya kitaifa. Vilevile, napenda kuwashukuru sana Wawekezaji, Mashirika yasiyo ya kiserikali na Wafadhili wetu kwa kutenga muda na kukubali kufika katika Mkutano huu kwani tunafahamu ya kuwa mnamajukumu mengi yakutekeleza. Kufika kwenu kumetufanya tujisikie kuwa **mmetuthamini** na **kutuheshimu**, na pia **mnatambua** umuhimu na mchango wa jamii katika uhifadhi wa Wanyamapori

Tanzania. Napenda kutoa Pole ya safari kwa Wawakilishi na Viongozi wa WMAs kwani natambua ya kuwa wengi wetu tumetoka mbali na tumechukua siku kadhaa hadi kufika hapa Arusha. Mwisho kabisa napenda kutoa shukrani kwa **Afisa Mtendaji Mkuu wa Muungano (Bw. George Wambura)** na wasaidizi wake kwa juhudi kubwa ya kuhakikisha kuwa mkutano huu unafanyika. **ASANTENI SANA**.

Ndugu Mgeni Rasmi na Washiriki wa Mkutano,

Muungano wa Jumuiya za Hifadhi ya Wanyamapori Tanzania **(CWMAC)** ni chombo cha **Juu** kinachoziunganisha Jumuiya zote za Hifadhi ya Wanyamapori Tanzania. Muungano huu ulianzishwa rasmi tarehe **22 Januari 2010** kama chombo **huru** kilichoundwa na Jumuiya anzilishi **14**. Aidha, Jumuiya zote **22** zilizofikia hadhi ya **"Authorized Association - AA"** ni wanachama wa Muungano.

Chombo hiki ni **Asasi ya kiraia** kinachotoa fursa kwa Jumuiya zote za Hifadhi ya Wanyamapori **kukutana**, **kubadilishana mawazo** na **uzoefu**, **kujadili** na **kupanga mambo yanayoadhiri wanachama wake** kwa kushirikiana na wadau.

Muungano huu unawajibu wa kuhakikisha kuwa:-

- Kunakuwepo usimamizi na uhifadhi endelevu katika maeneo ya WMAs,
- Kunakuwepo na mazingira mazuri ya uwekezaji kwenye WMAs,
- Kusaidia kuwepo Mipango mizuri ya usimamizi wa WMAs,
- Kuziunganisha na kuhakikisha kuwa WMAs zinamahusiano mazuri na wadau wengine,
- Kuziwakilisha na kutetea maslahi mbalimbali ya WMAs katika vyombo vinavyofanya maamuzi,
- Kusaidia upatikanaji wa masoko ya bidhaa zinazopatikana kwenye WMAs,
- Kutafuta fedha kwa ajili ya usimamizi endelevu wa raslimali za maliasili kwenye WMAs,
- Kufanya mambo yote yanayolenga kuleta ustawi wa WMAs.

Ndugu Mgeni Rasmi na Washiriki wa Mkutano,

Chimbuko la Mkutano huu ni kuongezeka kwa changamoto za uhifadhi na kibiashara ikiwa ni pamoja na mahusiano na ushikiano kati ya Wawekezaji na WMAs. Lakini kubwa zaidi, Mkutano huu umelenga katika kuwaleta pamoja Wawekezaji na WMAs kujadili changamoto za uwekezaji kwenye WMAs na kuandaa Mikakati ya kukabiliana nayo kwa kushirikiana na Wizara yako. Mkutano huu una umuhimu mkubwa kwani WMAs zinategemea shughuli za uwekezaji hususan katika Utalii wa picha na uwindaji wa kitalii ili kuweza kujiendesha, kufanya shughuli za doria na kutekeleza miradi ya maendeleo na kupunguza umaskini wa kipato kwa wanajamii. Inatarajiwa kuwa maazimio na mapendekezo yatakayopatikana yatawasilishwa Serikalini [Wizara ya Maliasili na Utalii (WMU)] na Taasisi nyinginezo za Serikali zitakazo bainishwa) ili kuweza kuboresha Taratibu, Miongozo, Kanuni na Sheria zinazohusu uwekezaji katika WMAs.

Ndugu Mgeni Rasmi na Washiriki wa Mkutano,

Kutokana na uzoefu mbalimbali kutoka kwa washiriki wa Mkutano, inatarajiwa kuwa mwisho wa Mkutano huu, changamoto mbalimbali zinazozuia uwekezaji bora katika WMAs zitabainishwa na kuundiwa Mikakati hususan katika maeneo ya Sera & Sheria, utaratibu wa ukusanyaji mapato na mgawanyo wa mapato, vibali na tozo mbalimbali na utaratibu mzima wa utoaji huduma katika shughuli za uwekezaji kutoka kwa WMAs na Serikali. Vilevile, baadhi ya migogoro kati ya WMAs na wawekezaji itapatiwa ufumbuzi na kuanzishwa upya mahusiano mazuri. Mwisho fursa mbalimbali za uwekezaji zitabainishwa ili kuweza kuleta manufaa kwa jamii zilizotenga maeneo yao kuanzisha WMAs.

Ndugu Mgeni Rasmi na Washiriki wa Mkutano,

Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na utalii, **Profesa Jumanne Magembe** naomba nikutaarifu kuwa wanajamii tunayo imani kubwa na Serikali ya **Dk. John Pombe Magufuli** kupitia Wizara yako. Hivyo napenda kukutaarifu kuwa kuna mambo ambayo ni **MAJIPU** na usipo yatumbua maantiki nzima ya Mkutano wetu inaweza kutoweka. Mambo hayo ni:-

- Wizara ya Maliasili na Utalii kuendelea kukusanya Fedha za utalii wapicha kwenye WMAs na kuingizwa kwenye Akaunti ya Pori la Akiba la Selous na hatimaye kuchelewa kurudishwa kwenye WMAs bila kujali WMAs zinajiendesha vipi.

- Fedha zinazotokana na Utalii wa Picha na Uwindaji wa kitalii kutumwa kwenye WMAs bila ya kuonesha mchanganua wa fedha husika. Mfano: - Jumla ya kiasi kilichokusanywa, idadi ya wageni, Idadi ya siku walizokaa, aina ya tozo, nk. Kutokana na mazingira ya fedha zetu zinavyotumwa tunashawishika kwa kiasi kikubwa kuwa Fedha zetu zinaliwa na baadhi ya wachache kwenye Wizara yako. Tunakuomba Mheshimiwa Waziri kuunda Tume shirikishi kufuatilia Fedha zetu kama zimekuwa zikitumwa kwa ufasaha na kuwachukulia hatua wahusika.

- Wizara ya Maliasili na Utalii kuendelea kukusanya Fedha za uwindaji wa kitalii kwenye WMAs na kuzipeleka Hazina na kiasi husika kuingizwa kwenye Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo imekuwa haipewi kiasi kinachoombwa Hazina (Budget cuts). Kila mwaka Fedha za uwindaji wa kitalii zimekuwa zikikatwa na kutumwa pungufu na bila ya kurejeshwa mwaka unaofuata.

- Wizara yako kushindwa kutekeleza **MAELEKEZO** ya Waziri wa Maliasili na Utalii (WMU) aliyemaliza muda wake, **Mhe. Lazaro Nyalandu** kwenye kikao cha wadau wote wa WMAs Tanzania kilichofanyika katika hoteli ya **Naura Springs tarehe 2 & 3 Julai 2015.**

- Mheshimiwa Waziri, tumetaarifiwa na Mkurugenzi Msaidi Maendeleo ya Wanyamapori (Bw. David Kanyatta) katika Mkutano wa Halmashauri kuu ya WMAs Tanzania tarehe 06 Januari 2016 kilichofanyika Morogoro, kuwa baada ya kikao cha mwisho cha wadau kupitisha rasimu ya Kanuni za WMA mwezi 21 Oktoba 2015, watendaji wa Wizara yako wameenda kukaa tena upya kuandaa rasimu ya mpya ya Kanuni hizo bila ya kuwashirikisha wadau na kuwa rasimu zote mbili zimewasilishwa kwako kwa maamuzi. Mheshimiwa Waziri utaratibu huu ni kinyume na dhana ya ushirikishwaji na hatuelewi kuna nini kimefichwa ambacho sisi kama wadau hatupaswi kukielewa. Kwa kifupi picha tunayoipata ni kuwa Wizara yako haipendi mabadiliko yanayolenga kuboresha WMAs kwa sababu tusizozifahamu na kutaka kuendelea kuwakandamiza

wananchi na kuchukua fedha zao. Hivyo, tunakuomba ufanye uchunguzi binafsi kuhusu haya tunayokueleza na kuwa makini na ushauri unaopewa na watendaji wako.

- Uwezo mdogo wa kifedha na upungufu wa raslimali watu wa kitengo cha CBC/WMA cha Idara ya Wanyamapori hivyo kushindwa kushughulikia mambo ya Kisera na Kisheria kwenye WMA kwa HARAKA ili kuepusha migogoro isiyokuwa ya lazima.
- Baadhi ya watumishi wa Wizara yako kushindwa kutekeleza wajibu wao ipasavyo hivyo kusababisha WMA kuingia kwenye migogoro. Mfano MBOMIPA jumuiya ambayo mimi ni Mwenyekiti imeshtakiwa Mahakama Kuu ya Tanzania kitengo cha Biashara na kudaiwa fidia na Kampuni za Kilombero Hunting Safaris Ltd na Wembere Hunting Safaris Ltd kwa Wizara yako kushindwa kutoa vibali vya Uwindaji wa kitalii kwa sababu ambazo zimesababishwa na Wizara yako.

Ndugu Mgeni Rasmi na washiriki wa Mkutano,

Mheshimiwa Waziri, wanajamii wamechoshwa na kukata tamaa kutokana na changamoto tajwa zinazosababishwa na Wizara yako hususan suala la ukusanyaji wa mapato na wengine wamefikia hatua ya kutaka kujitoa kwenye WMA. Kinyume na matakwa ya Sera ya Wanyamapori inayolenga kukasimu madaraka ya uhifadhi wa Wanyamapori kwa wanavijiji, wananchi bado wanaona WMAs si za kwao kwani kila kitu kinaamuli na Wizara ya Maliasili na utalii hii ikiwa ni pamoja na kukusanya na kurudishwa fedha za WMA kwa muda wanaotaka Wizara yako hivyo kuzuia uwezo wa kukua na uhuru wa kujiendesha. Mapinduzi yanahitajika katika kurudisha madaraka kwa wananchi ili waweze kunufaika na Ardhi waliyoitenga kwa ajili ya uhifadhi wa Wanyamapori na kupewa Haki ya matumizi ya Wanyamapori na Wizara yako. Hii ni pamoja na kushiriki katika shughuli za ulinzi wa Wanyamapori (Anti-poaching).

Ndugu Mgeni Rasmi na Washiriki wa Mkutano,

Mheshimiwa Waziri, jambo lingine la kushangaza ni kwamba WMAs hazijashirikishwa na kuwa si sehemu ya Mpango Mkakati wa kutokomeza Ujangili nchini (National Anti-poaching Strategy). Jambo hili si sawa kwani Vita ya ujangili hatuwezi kuishinda bila ya kushirikisha wananchi waishio pembezoni mwa Hifadhi za Taifa. Matharani, Pori la Selous lina ukubwa wa kilometa za Mraba 50,000 na halina fensi hivyo ni vigumu askari wa Pori hilo kuwa kila mahali na pia majangili wanaingia kupitia vijiji vinavyozunguka Pori hilo. Jumla ya WMA 7 zinazunguka pori hilo, hivyo ni jeshi jingine katika kuimarisha ulinzi wa Pori hilo endapo wananchi watanufaika na kuhamasika kutokana na uwepo wa WMAs hizo.

Ndugu Mgeni Rasmi na washiriki wa Mkutano,

Mheshimiwa Waziri, wenzetu katika nchi za jirani hususan Namibia na Kenya, serikali haichukui kiasi chochote cha fedha (inaachie 100% fedha zote zinazotokona na shughuli za utalii kwenye maeneo hayo) katika maeneo ya hifadhi ya Jamii yenye muundo sawa na WMAs za kwetu hapa Tanzania. Vilevile, Serikali husika zimeachia mamlaka Jumuiya zao kukusanya fedha na kujiendesha na hivyo kupelekea wananchi kuhamasika na ujangili kupungua katika maeneo yao. Tunaomba Wizara yako ijifunze na kuchukua hatua za **HARAKA** ili kuweza kunusuru Wanyamapori wetu.

Ndugu Mgeni Rasmi na washiriki wa Mkutano,

Nisingependa kuwachosha kwa Hotuba ndefu kwani kazi yangu ni kuwakaribisha na pia baadhi ya mambo mengine yanayotukera yatawasilishwa kwa kifupi na mwakilishi wa Wawekezaji. Lakini pia katika siku mbili za Mkutano wetu kuna mambo mengi ya kujadili. Hivyo basi tunakuomba Mheshimiwa Waziri kwa mambo haya machache tuliyokujulisha usimamie haki na utupe moyo sisi wanavijiji katika uhifadhi wa wanyamapori kwenye maeneo yetu na hifadhi zinazotuzunguka.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA NA KARIBUNI SANA.